# NDOA YA KULAZIMISHWA

## Ndoa ya Kulazimishwa ni nini?

Ndoa ya kulazimishwa ni ndoa ambayo mtu mmoja au wote wawili hawakubaliani kwa hiari (ridhaa) kwa ndoa na ambapo aina fulani ya shinikizo (shurutisho) inahusika.

Shinikizo hili linaweza kuchukua sura nyingi na linaweza kuwa la kimwili, kihisia, kisaikolojia na kifedha. Inaweza kujumuisha udanganyifu, vitisho, mpango wa kudhuru au unyanyasaji.

Mara nyingi kuna shinikizo kubwa la kufuata matakwa ya familia na jamii. Shinikizo linalomlazimisha mtu kuingia kwenye ndoa si lazima lielekezwe dhidi ya mtu huyo na linaweza kujumuisha mazingira ambayo vitisho vinatolewa kwa mtu huyo au watu wengine ikiwa hawakubaliani na ndoa hiyo.

Ndoa ya kulazimishwa pia inaweza kufanyika pale ambapo mtu hawezi kukubaliana kwa hiari yake, kwa mfano, watoto au watu wazima wenye matatizo ya akili.

Ndoa ya kulazimishwa si sawa na ndoa ya kupangwa. Katika ndoa ya kupangwa, pande zote mbili zinaridhia ndoa hiyo.

## Je, kuna haki/ulinzi gani ili kuwalinda watu dhidi ya ndoa za kulazimishwa?

Nchini Scotland, sheria inatoa ulinzi wa kiraia na wa jinai dhidi ya ndoa ya kulazimishwa.

### Kosa la Jinai

Ni kosa la jinai Scotland kulazimisha mtu kuolewa bila makubaliano yao kamili na ya hiari (ridhaa). Hii ina maana ni kosa la

jinai kutumia vitisho, kulazimisha au vurugu ya kulazimisha mtu mwingine kufunga ndoa.

Pia ni kosa la jinai kumdanganya mtu au kutumia aina yoyote ya udanganyifu kumfanya aondoke Uingereza na kusafiri kwenda nchi nyingine, kwa nia ya kumlazimisha mtu huyo kufunga ndoa.

Sheria inatumika hata kama shinikizo lolote litatumika nje ya Uingereza na au kwa raia wa Uingereza, au mtu anayeishi Scotland. Hii ina maana kwamba bado litakuwa ni kosa chini ya sheria ya Scotland na linaweza kuhukumiwa katika mahakama za Scotland.

Adhabu hizo ni pamoja na kifungo au faini, au zote mbili.

### Haki za wanawake wanaporipoti polisi

Kesi nyingi za ndoa za kulazimishwa haziripotiwi. Kunaweza kuwa na vikwazo vingi vinavyofanya iwe vigumu kwa mtu kuzungumza juu ya kile kinachotokea. Ni muhimu kujua kwamba una haki unaporipoti polisi ndoa ya kulazimishwa, au aina nyingine za uhalifu. Baadhi ya mambo ambayo mwanamke anaweza kuomba ni pamoja na:

- Unaweza kuomba afisa wa kiume au wa kike, ikiwa hii itakufanya ujisikie vizuri zaidi. Hii inapaswa

kuheshimiwa, isipokuwa kuna hali za kipekee.
- Unaweza kuuliza kutoa taarifa mahali fulani unapojisikia vizuri.
- Unaweza kuomba kuwa na mtu pamoja nawe kwa usaidizi (mradi tu yeye si shahidi).
- Unaweza kuomba kupewa askari kanzu ikiwa una wasiwasi kuhusu askari kuja nyumbani kwako na wanaoweza kumwona.
- Unaweza kuomba mkalimani na nyaraka fulani kutafsiriwa ikiwa zinahitajika kwa ajili ya ushiriki wako katika uchunguzi
- Una haki ya kupewa usaidizi, ikiwa ni pamoja kupata huduma za ukalimani (hata kama huhitajiki huripoti polisi).

**<u>Ulinzi wa Raia</u>**

Sheria ya kiraia ya Scotland pia inatoa ulinzi dhidi ya ndoa za kulazimishwa.

Sheria ya Ndoa ya Kulazimishwa (Ulinzi na Mamlaka) (Scotland) ya 2011 ilianzisha Amri Dhidi ya Ndoa za Kulazimishwa (FMPO).

Amri za aina hii hutolewa na mahakama za kiraia, sio mahakama za makosa ya jinai.

FMPO inaweza kuendeshwa kwa wakati mmoja na uchunguzi wa jinai au kesi za jinai.

## Je, FMPO Inaweza Kufanya Nini?

FMPO imeundwa kulingana na mahitaji ya mtu binafsi. Agizo linaweza:
- Kuzuia ndoa ya kulazimishwa kufanyika
- Kuchukua hatua kwa ajili ya ulinzi wako ikiwa ndoa ya kulazimishwa imekwishafanyika.
- Kujumuisha mambo kama vile kumpeleka muathirika mahali pa usalama, na kuwasilisha hati, kama vile pasipoti, mahakamani.
- Kutolewa notisi ya papo kwa hapo ya ulinzi wa haraka (inayojulikana kama "amri ya muda").

- Kutoa shinikizo nje ya, na vile vile ndani, Scotland.
- Kutumika kwa mtu ambaye analazimisha au kujaribu kulazimisha mtu kufunga ndoa ya kulazimishwa, na kwa watu wengine ambao wanaweza kumsaidia au kumtia moyo mtu anayelazimisha.

Ni kosa la jinai kuvunja FMPO, na polisi wanaweza kumkamata mtu kwa kosa hilo bila kibali.

Mahakama itaangalia kama amri hiyo ni muhimu ili kumlinda mtu dhidi ya ndoa ya kulazimishwa.

## Ushauri na Usaidizi Uliopo

Kituo cha Haki za Wanawake cha Scotland hutoa taarifa za kisheria, uwakilishi na usaidizi wa utetezi bila malipo kwa wanawake walioathiriwa na unyanyasaji Scotland.
- Simu ya Usaidizi: 08088 010 789
- Tovuti: https://www.scottishwomensrightscentre.org.uk/

**Simu ya Usaidizi dhidi ya Unyanyaswaji Majumbani na Ndoa za Kulazimishwa**: 0800 027 1234, (wazi masaa 24, simu ni bure na zenye usiri)

**Kitengo cha Ndoa za Kulazimishwa**, wazi jumatatu hadi Ijumaa, saa 3 asubuhi hadi 11 jioni, huweza kutoa ushari wa kitaalam wa nini cha kufanya:

- 020 7008 0151
- Nje ya Nchi: +44 (0)20 7008 0151
- Nje ya masaa ya kazi: 020 7008 1500 (ulizia Global Response Centre).
- Tovuti: fmu@fco.gov.uk

**Simu ya Msaada dhidi ya Mgogoro wa Ubakwaji Scotland**: 08088 01 03 02 (saa 11 jioni-usiku wa manane).

**Usaidizi na Habari Kuhusu Unyanyasaji wa 'Heshima' na Ndoa ya Kulazimishwa:**

- Shakti Women's Aid – 0131 475 2399
- Hemat Gryffe Women's Aid – 0141 353 0859
- Amina, MWRC – Simu: 0808 801 0301